

GRADE 4 KISWAHILI END TERM 1

1. Andika wingi wa maneno yafuatayo.

- (a) Chura - _____
- (b) Mtoto - _____
- (c) Ndege - _____
- (d) Mdudu - _____
- (e) Nyuki - _____

2. Tunga sentensi ukitumia nomino zifuatazo.

- (a) Rafiki _____

- (b) Shule _____

3. Piga mstari kitenzi katika sentensi hizi.

- (a) Wanafunzi wanaandika insha.
- (b) Mama anapika chakula kitamu.
- (c) Maria anacheza na paka.

4. Chagua kiwakilishi katika kundi hili la maneno.

- (a) nguo, dada, yeye, Ali _____
- (b) mbwa, lima, cheka, wewe _____
- (c) nyinyi, Nyeri, lia, ugali _____

5. Maamkuzi na maagano haya hutumiwa wakati upi?

- (a) Habari yako? _____
- (b) Masalheri _____
- (c) Alamsiki _____
- (d) Siku njema _____
- (e) Kwaheri _____

6. Tegua vitendawili vifuatavyo:-

- (a) Nyumba yangu haina mlango _____
- (b) Atolewapo nje hufa _____

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Kazungu anaishi katika kijiji cha Kaloleni. Yeye na dada yake Kadzo wanapendana sana. Ni kawaida kwa Kazungu kuamka kabla ya Kadzo. Anapoamka huchukua kiberiti na kuwasha taa ya kibatari. Kazungu anajua kukoka moto akitumia makumbi ya nazi.

Yeye hujikaza kupika kahawa na kaimati kwa kiamshakinywa. Baada ya kuoga, Kazungu huvaa suruali ya zambarau na sweta ya buluu. Yeye hukimbia kama swara kufungulia ng'ombe wakati mwingine Kadzo humfuata karibu karibu kama kivuli. Yeye hushinda malishoni siku ya Jumamosi.

- (a) Kazungu anaishi wapi? _____
- (b) Dadake Kazungu anaitwa nani? _____
- (c) Ni nani huamka mbele ya mwingine? _____
- (d) Kazungu akiamka huchukua kiberiti na kuwasha taa ya kibatari. Taa ya kibatari ni taa ya aina gani? _____
- (e) Kazungu na Kadzo hula _____ kama kiamshakinywa.
- (f) Ni nani hujikaza ili apike kiamshakinywa? _____
- (g) Kazungu huvaa nini baada ya kuoga? _____
- (h) Kazungu hukimbia kama nini ili kufungulia ng'ombe? _____
- _____
- (i) Kazungu na Kadzo hufanya nini siku ya Jumamosi? _____
- _____
- (j) Hadithi hii inatufundisha nini? _____